WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA, NA MAFUNZO YA UFUNDI.

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA.

SHULE YA SEKONDARI MADUNDA.

S.L.P 654,

NJOMBE.

SIMU 0620547837

Tarehe……2021

KUMB Na: MSS/LDW/J.IN/2020

JINA LA MWANAFUNZI……

SHULE ATOKAYO……..

S.L.P ……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MADUNDA WILAYA YA LUDEWA MKOA WA NJOMBE MWAKA 2020.

1.0: UTANGULIZI:

Nina furahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020.Shule ya sekondari Madunda ipo katika Wilaya ya Ludewa , kata ya Mawengi ,kijiji cha Madunda umbali wa km 55 kutoka Wilayani barabara iendayo Njombe. Usafiri upo wa mabasi na pikipiki/boda boda.

Shule itafunguliwa tarehe 06/01/2020 Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare na vifaa vyote vilivyoagizwa. Mwisho wa kupokea wanafunzi ni tarehe 13/01/2020

2.0: MAMBO YA KUZINGATIA.

2.1: SARE ZA SHULE:

- **WAVULANA**:- Suruali mbili za rangi ya kijani , ni lazima ziwe za heshima.
    - Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
    - Viatu vya ngozi ,vyeusi vya kamba visiwe buti wala kisigino kirefu.
    - Soksi nyeusi jozi mbili
    - Masweta mawili (2) ya rangi ya bendera ya taifa
    - T-sheti ya rangi ya bluu kwa ajili ya kazi za nje yenye shingo ya duara na isiwe na Maandishi yoyote yale.
- Fulana nyeupe mbili (2) (singland) pamoja na chupi 4 au boxer 4.
- Chandarua kimoja kwa ajili ya kuzuia mbu.

- **B. WASICHANA**: -:- Suruali mbili za rangi ya kijani , ni lazima ziwe za heshima.
- Visoro vyeupe viwili vya malinda ya kukimbizana vyenye urefu wa kutosha kufunika Makalio .
- Viatu vya ngozi ,vyeusi vya kufunga na kamba visiwe na kisigino kirefu viatu vya Plastiki haviruhusiwi
- T-sheti ya rangi ya bluu kwa ajili ya kazi za nje yenye shingo ya duara na isiwe na Maandishi yoyote yale.
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Sweta rangi ya bendera ya Taifa (masweta mawili)
- Hijab nyeupe (kwa wanafunzi wa kiislamu tu).
- Nguo za ndani chupi, undersketi na taiti (Dazani moja)
- Chandarua kimoja kwa ajili ya kuzuia mbu

NB: **MWANAFUNZI ATAKAYE SHONA SURUALI RANGI TOFAUTI NA KITAMBAA TULICHO AMBATANISHA KATIKA BARUA HII ATARUDISHWA ILI AKASHONE NYINGINE.**

C: SARE ZA MICHEZO: Sare za michezo kwa shule hii ni:

- Trakisuti ya rangi ya dark bluu kwa wavulana na wasichana
- Raba

2.2: VIFAA VYA DARASANI:

- Bunda la karatasi nyeupe (A4)
- Daftari kubwa 11(counter book Quire 3.)
- Daftari ndogo za kati 11 (pg 80)
- Kalamu za kutosha muhula (za wino na za risasi)
- Mkebe wa hesabu (Mathematical set wenye vifaa vyake vyote ndani).
- Dictionary ya Kingereza kwa Kiswahili
- Mkoba wa kubebea daftari (begi)

2.3: MAHITAJI MENGINE YA KIBINADAMU:

a) Vifaa vya usafi kwa Wanafunzi wote (Wakiume/Wakike):

(i) Ndoo ya lita 10 (1) moja

(ii) Ufagio wa chelewa mmoja (1).

(iii) Jembe jipya lenye mpini (1)

(iv) Kwanja lililonolewa moja.

2.4. Aidha shule inatoa huduma ya uji na chakula cha mchana hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kuleta mahindi debe mbili, maharage kilo 10 na sh 35,000/=kwa muhula kwa ajili ya sukari,kuni ,kusaga na kumlipa mpishi.

3.0: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu , Sayansi , Teknolojia , na Mafunzo ya Ufundi , yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

3.1

- Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni Jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
    - Kutunza usafi wa Mwili , mavazi na mazingira ya shule
    - Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
    - Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
    - Kutunza mali za umma.

3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kukusababishia kufukuzwa au kusimamishwa shule:

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi ,cocaine, mirungi, kubeli nk
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) kuwa mjamzito/kupata mimba/kusababisha mimba

i) Kuoa au kuolewa

j) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

k) Kukataa adhabu kwa makusudi

l) kuwa na simu ya mkononi

4.0 **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapofika shuleni.

b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai .

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule.

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

……..

ISMAEL R.MLIMBILA

MKUU WA SHULE

KWA MAWASILIANO :MKUU WA SHULE – 0764 516 626

SHULE – 0768 719 629

NB: Pia kuna huduma ya Hosteli kwa Wanafunzi wa jinsi zote,kwa wazazi wanaohitaji watoto wao wakae hosteli wawasiliane na uongozi wa shule kwa namba za hapo juu kuhusu utaratibu wa hosteli.

(FC)

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA , NA MAFUNZO YA UFUNDI.

SHULE YA SEKONDARI MADUNDA.

FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA , KANUNI, NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI.

1. Mimi ……Mzazi/Mlezi nimekubali mtoto wangu ……asome katika shule ya sekondari Madunda kuanzia tarehe……
2. Ninaahidi kumpatia mahitaji /vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua ya kujiunga na shule.

3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria zote za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii katika masomo na kazi za kujitegemea.
4. Anuani yangu ya kudumu ni,
   ……
   ……..
   ……..
   SIMU:…….
5. Sahihi……Tarehe…….

(FA)

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI MADUNDA

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MADUNDA

SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi ……msichana/mvulana nimekubali kuingia Kidato cha ……..katika shule ya Sekondari Madunda kama Mwanafunzi wa (Kutwa/Hosteli)…….. tangu tarehe……nitafika bila kukosa.
2. Nitatii sheria na kanuni zote , na nitakuwa Mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea.

Sahihi ya mwanafunzi……. Tarehe ……..

MAONI YA MZAZI/MLEZI KUHUSU MTOTO

1. Tafadhali eleza endapo kuna tatizo, jambo au tabia yoyote ambayo mkuu wa shule anapaswa kufahamu juu ya mtoto wako.
   ……
   ……
   ……
   ……
   …….
2. UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI
   Nimesoma maelezo yote na kuyaelewa vema. Hivyo nakubali kutekeleza maagizo yote kikamilifu. Pia ntahakikisha mwanangu anafuata na kuzingatia taratibu zote za shule.
   Jina la Mzazi/Mlezi ……sahihi……..tarehe……

`